# JARIDA LA RS RUVUMA
# TOLEO LA OKTOBA 2024











# KARIBU MKOA WA RUVUMA

Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya Jarida hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Mwandishi kwa maandishi.

## JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO LA OKTOBA 2024

Jarida limehaririwa na **Albano Midelo** wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

## TAHARIRI

Wapendwa wasomaji wetu ninayoheshima kubwa kuwaalika katika Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kusoma habari na makala mbalimbali ambazo zinakuwa zinachapishwa na jarida hili.
Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikali kuhakikisha kila mwezi GCU Mkoa na Halmashauri zake zinachapisha jarida ili kutangaza shughuli mbalimbali zinazofanywa na serikali ikiwemo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, mahusiano na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma na namna viongozi wa ngazi ya Wilaya,Mkoa na kitaifa wanavyofanya ziara za kuzungumza na wananchi,kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Furahia kusoma

## BILIONI 14.5 KUSAMBAZA UMEME VITONGOZI 135 RUVUMA



Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inatekeleza mradi wa shilingi bilioni 14.56 wa kusambaza umeme katika vitongoji 135 Mkoani Ruvuma utakaonufaisha Kaya 4,455.

Mhandisi Msimamizi wa Miradi ya Umeme REA Kanda ya Kusini, Mhandisi Deogratius Nagu amebainisha hayo mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali

Ahmed Ahmed wakati wa kumtambulisha Mkandarasi aliyeshinda zabuni ya kutekeleza mradi huo Kampuni ya CCC International Nigeria LTD.

“Katika kuhakikisha maendeleo yanafika kote nchini, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais  Dkt. Samia Suluhu Hassan imeidhinisha kiasi cha shilingi bilioni 14.56 kitumike kutekeleza mradi wa kusambaza umeme katika vitongoji 135 Mkoani Ruvuma,” alisema Mhandisi Nagu.

Akizungumza wakati wa utambulisho wa Mkandarasi huyo, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Ahmed ameipongeza REA kwa kuendelea kutekeleza dhamira ya Rais Dkt. Samia kwa vitendo na amesisitiza Mkandarasi huo kuhakikisha anakamilisha mradi kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

Mkoa wa Ruvuma una vitongoji 3,693 kati ya hivyo , vitongoji 1,973 vimefikishiwa umeme ambayo ni sawa na asilimia 53 na kwamba vitongoji 135  vitapata umeme kupitia mradi huo. unaotekelezwa katika majimbo tisa mkoani Ruvuma.

## WALIOPEWA MAENEO  HIFADHINI WATAKIWA KUYAENDELEZA




Waziri wa Maliasili na Utalii Balozi, Dkt. Pindi Chana amewataka wawekezaji waliopewa maeneo katika maeneo ya uhifadhi kuwekeza na kuyaendeleza vinginevyo taratibu za kisheria zitachukuliwa.

Ameyasema hayo alipotembelea na kukagua miradi mbalimbali ya kimkakati katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere Mkoani Ruvuma.

"Kuna watu wameshikilia maeneo katika maeneo yetu ya Uhifadhi, hakuna mtu anaendeleza, hapo unakosesha ajira kwa vijana, Mapato kwa Serikali, hilo hatutaruhusu, Wale waliopewa maeneo katika hifadhi wawekeze lasivyo taratibu za kisheria zitachukuliwa", Alisema.

Akiwa katika ziara hiyo, Balozi Chana amekagua lango la Kitalii la kisasa lakuingilia hifadhini hapo, Mradi wa ujenzi wa kiwanja cha Ndege, Nyumba ya wageni na Ujenzi wa Nyumba za watumishi.

Sanjari na hayo, amebainisha kuwa Nchi ya Tanzania ina vivutio vingi vya Utalii na maeneo ya Wanyama ambapo shughuli mbalimbali za Utalii kama vile Utalii wa uwindaji, upigaji picha na Utalii wa maji.

Ameeleza kuwa Wizara na Jeshi la Uhifadhi limejipanga kuhakikisha rasilimali za Nchi zinalindwa na ametoa rai kwa Wananchi kufuata sheria, kuacha kuchoma moto na kuingiza Mifugo katika Hifadhi.

Kwa Upande wake Kamishna Msaidizi Uhifadhi, Hifadhi ya Taifa ya Nyerere Ephraim Mwangomo amesema ujenzi wa Miundombinu ya hifadhi hiyo ikiwemo lango la kisasa, uwanja wa ndege na Nyumba za watumishi umegharimu Tsh. Bilioni 2.1.

Amewaomba wawekezaji kuja kuwekeza katika hifadhi ya Taifa ya Nyerere akieleza kuwepo kwa idadi kubwa ya watalii wanaotoa fursa kwa wawekezaji hususani katika eneo la ujenzi wa Nyumba za wageni.

Sekta ya Maliasili na Utalii inachangia pato la Taifa kwa asilimia 17.5 na fedha za kigeni kwa asilimia 25

## MAADHIMISHO YA JUMA LA ELIMU YA WATU WAZIMA KIMKOA



Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Mary Makondo alipotembelea moja ya mabanda kutoka Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma katika maadhimisho ya Juma la elimu ya watu wazima ambalo kimkoa yamefanyika Mbambabay wilayani Nyasa.

Kau;imbiu ya mwaka huu ni Ujumuishi katika elimu bila ukomo kwa ujuzi ,ustahimilivu ,amani na maendeleo



Maafisa Elimu Watu Wazima katika Halmashauri zote mkoani Ruvuma wameagizwa kuhakikisha wanasimamia uwepo wa madarasa ya kisomo na SEQUIP katika kila Kata.

Agizo hilo limetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed katika hotuba iliyosoma kwa niaba yake na Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Mary Makondo katika kilele cha maadhimisho ya Juma la Elimu kimkoa ambayo yamefanyika Mbambabay wilayani Nyasa.

“Niwaombe wananchi kujiunga kwa wingi katika madarasa hayo kama ilivyo dhamira ya Rais wetu Dkt.Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kila kijana wa kike aliyekatisha masomo anarejeshwa shuleni’’,alisisitiza Kanali Abbas.

Kupitia maadhimisho hayo,Mkuu wa Mkoa amewaagiza wakurugenzi wote wa Halmashauri na maafisa Elimu Msingi na Sekondari wahakikishe kuwa elimu ya watu wazima inatiliwa mkazo kwa kuweka mikakati mizuri ili iweze kutekelezwa kikamilifu.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi kwenye maadhimisho hayo,Afisa elimu Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa

Ruvuma Mwl.Mathias Tilia amesema Mkoa kwa kushirikiana na Taasisi ya elimu Tanzania unatekeleza program kwa wasichana waliokatisha masomo ya sekondari ambapo hadi sasa jumla ya wanafunzi 228 wananufaika na mradi huo.

Tilia amesema Mkoa wa Ruvuma una jumla ya vituo 70 vya elimu ya msingi kwa Watoto walioikosa (MEMKWA) vyenye jumla ya wanafunzi 317 kati yao wavulana 231 na wasichana 186 na kwamba wanafunzi hao walikosa fursa ya kupata elimu katika mfumo rasmi kutokana na changamoto mbalimbali za kimaisha.

Ameongeza kuwa Mkoa wa Ruvuma una vituo vitano vya ufundi stadi ambavyo hutoa mafunzo kwa wanafunzi waliomaliza elimu ya msingi na sekondari katika fani za useremala,ushoni,udobi na upishi na kwamba vituo hivyo vinawapa ujuzi wa stadi mbalimbali vijana ili kuwawezesha kukabiliana na changamoto za kimaisha.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Nyasa Mheshimiwa Peres Magiri akizungumza kwenye maadhimisho hayo yenye kaulimbiu ya ujumuishi katika elimu bila ukomo kwa ujuzi,ustahimilivu,amani na maendeleo,amesisitiza wananchi kuendelea kupata elimu kupitia mfumo usiokuwa rasmi kwa kuwa elimu haina mwisho.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Mary Makondo akikagua maoja ya mabanda katika maadhimisho ya Juma la elimu ya watu wazima kimkoa ambayo yamefanyika Mbambabay wilayani Nyasa

# SERIKALI ILIVYOWEKEZA KATIKA SEKTA YA AFYA MBINGA



WANANCHI wa vijiji vilivyopo katika Halmashauri ya wilaya Mbinga mkoani Ruvuma,wamesisitizwa kutumia zahanati,vituo vya afya na Hospitali zinazojengwa na Serikali kwenda kufanya uchunguzi wa afya zao na kupata huduma za matibabu.

Rai hiyo imetolewa kwa nyakati tofauti na Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mbinga Dkt Seleman Jumbe,wakati wa ziara yake ya kutembelea vituo vya kutolea huduma za afya ikiwemo ujenzi wa mradi wa wodi ya wanawake,watoto na wanaume yanayojengwa katika Hospitali ya Halmashauri iliyopo kijiji cha Kigonsera wilayani Mbinga.

Alieleza kuwa,wananchi wanatakiwa kuhakikisha wanatumia vituo na Hospitali hizo kupata huduma kwa kuwa fedha zinazotumika kutekeleza miradi hiyo zinatolewa na Serikali yao na wanapaswa kujivunia na uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali.

Dkt Jumbe alisema kuwa,Serikali imetoa Sh.milioni 850 kati ya hizo Sh.milioni 500 zimepangwa kutumika kujenga wodi tatu ambazo ujenzi wake upo hatua ya kufunga milango,madirisha na kuweka malumalu na Sh.milioni 35 kwa ajili ya kununua vifaa tiba.

“Mbali na fedha hizo Mheshimiwa Rais Samia ametupatia fedha nyingine Sh.milioni 300 ili kujenga jengo la upasuaji,kwa sasa tupo katika hatua za manunuzi ili kumpata mzabuni kwa ajili ya kuanza ujenzi”alisema Dkt Jumbe.

Alisema,mpango wa Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kupitia Halmashauri ya wilaya Mbinga ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma za matibabu kwenye maeneo yao ili kuwaondolea adha ya kwenda mbali kufuata huduma za afya.

Alisema,Hospitali ya Halmashauri kwa sasa inahudumia zaidi ya wakazi 60,000, hata hivyo matarajio yao majengo mapya yatakapokamilika idadi ya wananchi itaongezeka kutokana na uwepo wa huduma muhimu ikiwemo za upasuaji.

Kwa mujibu wa Dkt Jumbe,Halmashauri ya wilaya Mbinga kuna vituo 8 vya afya,lakini mkakati uliopo kujenga vituo vingine kwa kila kata na wameanza kujenga vituo viwili katika kata ya Linda na Mkumbi ambapo ujenzi wake unaendelea vizuri.

Kwa upande wake Mganga mfawidhi wa Hospitali ya Halmashauri ya wilaya Mbinga Dkt Salum Bundala,amemshukuru Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuleta fedha zilizowezesha kujenga majengo matatu ya wodi ya akina mama,wanaume,watoto na jengo la utawala ambayo yakikamilika yataondoa adha iliyopo ikiwemo ukosefu wa wodi ya kulaza wagonjwa.




Baadhi ya majengo katika hospitali ya Halmashauri ya wilaya ya Mbinga

# SERIKALI KUBORESHA HUDUMA YA MAMA NA MTOTO



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amebainisha kuwa Serikali imedhamiria kuboresha huduma za afya ya uzazi na Watoto Nchini kwa lengo la kupunguza na kumaliza tatizo la vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga vinavyoweza kuzuilika.

Ameyasema hayo alipoongoza Kikao cha makabidhiano na majadiliano ya mwendelezo wa mfumo wa usafirishaji wa dharura kwa akina mama wajawazito, waliojifungua na watoto wachanga(M-mama) kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea.

"Serikali ya awamu ya sita inayodhamira ya dhati ya kuboresha huduma za afya ya uzazi na Mtoto Nchini kwa lengo la kupunguza au kumaliza tatizo la vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga vinavyoweza kuzuilika"

Amesisitiza kutoa kipaumbele kwa Rufaa kwa wazazi na Watoto wachanga na halmashauri kusimamia Mfumo wa M-mama kwa kuhakikisha Magari ya Wagonjwa yapo tayari wakati wote na kuweka uratibu mzuri kwa madereva ngazi ya jamii.

Amewaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha Halmashauri zimetenga bajeti zitakazowezesha shughuli za Rufaa kwa Mfumo wa M-mama kwa kila mwaka wa fedha.

Amewaagiza kuhakikisha vituo vyote vinavvyotoa huduma za Afya vinatumia mfumo wa M-mama ili taarifa za wanaopewa rufaa zifahamike na kuhakikisha wote wanaohusika kuratibu Mfumo wa M-mama wanatekeleza wajibu yao kwa weledi.

Sanjari na hayo Kanali Ahmed amesisitiza kujitahidi kudhibiti na kuwa makini na upotoshaji wowote unaofanywa ili malengo ya Serikali yasihujumiwe.

Kwa upande wake Muuguzi Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Hilda Ndambalilo amesema hadi sasa mfumo wa M-mama umewezesha kusafirisha jumla ya wagonjwa 1,938 kati yao akinamama wajawazito 1,664 na Watoto wachanga 274.

Naye Mratibu wa Mfumo wa M-mama Nyanda za Juu Kusini kutoka Pathfinder Magdalena Mwaikambo ameeleza kuwa Mfumo wa M-mama umeweza kupunguza ucheleweshwaji wa usafirishaji wa rufaa za kina mama na watoto wachanga wenye uhitaji.

M-mama ni mfumo wa usafirishaji wa dharura wa akinamama wajawazito, waliojifungua ndani ya siku 42, na watoto wachanga ndani ya siku 28.



Baadhi ya washiriki kutoka katika Halmashauri zote nane za Mkoa wa Ruvuma wakiwa kwenye kikao cha makabidhiano ya mwendelezo wa mfumo wa usafirishaji wa dharura kwa akina mama wajawazito (M-mama) kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed

## SERIKALI IMELETA MAGARI MENGI YA WAGONJWA RUVUMA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesema serikali imefanyya juhudi kubwa za kuleta magari ya kubeba wagonjwa (Ambulance) ili kuimarisha huduma za rufaa za wagonjwa hasa mama na mtoto.

Kanali Abbas amesema hayo wakati anazungumza katika makabidhiano ya mwendelezo wa mfumo wa usafirishaji wa dharura kwa akina mama wajawazito (M-mama) kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea.

Amesema hivi sasa Mkoa wa Ruvuma una jumla ya magari ya kubeba wagonjwa 21 kati ya hayo magari 15 ni mapya kabisa.

“Natambua kuwa kiuhalisia magari ya kubebea wagonjwa yaliyopo hayawezi kutosheleza mahitaji ya kusafirishia rufaa kutoka pande zote za Mkoa wetu kutokana na sababu mbalimbali,hivyo pengo hili litaendelea kuzibwa kwa kuwatumia madereva ngazi ya jamii ambao wamesaini mikataba katika Halmashauri zetu’’,alisisitiza Kanali Abbas.

Amesema serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto lengo likiwa ni kupunguza na kumaliza tatizo la vifo vinavyotokana na uzazi na vifo vya Watoto wachanga vinavyozuilika.

Hata hivyo Mkuu wa Mkoa ameziagiza Halmashauri zote mkoani Ruvuma kusimamia mfumo wa M-mama kwa kuhakikisha magari ya wagonjwa yanakuwa

tayari wakati wote na kuhakikisha kunakuwa na utaratibu mzuri wa madereva ngazi ya jamii na kusimamia kuharakisha malipo yao kulingana na mikataba.

Kanali Abbas amewaelekeza wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha Halmashauri zimetenga bajeti zitakazowezesha utekelezaji wa shughuli za rufaa kila mwaka na kuendelea kuweka fedha kwenye akaunti kuu ya Taifa ya m-mama iliyoanzishwa na serikali.

Naye Muuguzi Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Hilda Ndambalilo ameutaja mfumo wa M-mama kuwa ni mfumo wa usafirishaji wa dharura wa akinamama wajawazito waliojifungua ndani ya siku 42 na Watoto wachanga wa siku 0 hadi 24.

Amesema katika mfumo huo ambao ulizinduliwa mkoani Ruvuma Mei 2023,hadi sasa umewezesha kusafirisha jumla ya wagonjwa 1,938 kati yao akinamama wajawazito 1,664 na Watoto wachanga 274.

## RUVUMA YAZALISHA ZAIDI YA TANI 23,000 ZA KAHAWA



Mkoa wa Ruvuma katika msimu wa mwaka 2024/2025 hadi kufikia Septemba mwaka huu umefanikiwa kuzalisha tani 23,910,703 za kahawa kavu.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed wakati anazungumza kwenye maadhimisho ya siku ya kahawa duniani ambayo kimkoa yamefanyika katika Kijiji cha Liganga wilayani Songea.

Hata hivyo amesema katika msimu huu,Mkoa wa Ruvuma unatarajia kuzalisha tani 25,000 ambapo hadi sasa Mkoa wa Ruvuma unashika nafasi ya pili katika uzalishaji wa kahawa Tanzania baada ya Kagera.

Amesema katika msimu wa mwaka 2023/2024 Mkoa wa Ruvuma ulizalisha zaidi ya tani 22,000 za kahawa kavu na kwamba katika kuendeleza zao la kahawa ,Bodi ya kahawa imeweka malengo makuu matatu.

Ameyataja malengo hayo kuwa ni usajili wa wakulima wote wa kahawa ili kuwa na mpango sahihi wa kuwahudumia,utoaji wa miche bora kahawa ambapo kwa mwaka huu tayari miche 3,190,000 itatolewa bure kwa wakulima na mpango wa ufufuaji wa mashamba ya miti ya kahawa iliyozeeka.

"Hali ya uzalishaji wa zao kahawa katika Mkoa wa Ruvuma bado una changamoto nyingi,uzalishaji kwa wakulima wengi ni mdogo, wakulima waelimishwe kuwekeza vizuri katika maeneo yao na ufanyike uhamasishaji wa kupanua mashamba na kuanzisha mashamba mapya'',alisema.

Mkuu wa Mkoa amemshukuru Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan anavyowekeza kwenye kilimo ikiwemo zao la kahawa ambapo hivi karibuni alitembelea shamba la kahawa la AVIV wilayani Songea.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Nyasa Mheshimiwa Peres Magiri akizungumza kwa niaba ya wakuu wa wilaya wa Mkoa wa Ruvuma kwenye maadhimisho hayo ametoa rai kwa wakulima kuuza kahawa yao kwa njia ya mnada ili kupata bei nzuri kulingana na bei ya soko.

Amesema upatikanaji wa mbolea ya ruzuku umesaidia katika uzalishaji wa zao la kimkakati la kahawa mkoani Ruvuma hivyo wananchi wanapata faida kubwa.

Kaulimbiu ya siku ya maadhimisho ya siku ya kahawa Duniani mwaka huu ni Tunza mazingira kwa kilimo endelevu.

## MAHAKAMA ILIVYODHAMIRIA KULINDA MAADILI



Jaji Mfawidhi, Mahakama Kuu ya Tanzania kanda ya Songea Mheshimiwa James Karayemaha amesema Mahakama imedhamiria kusimamia kwa uzito suala la

maadili ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua mbalimbali za uwajibikaji kwa maafisa wa Mahakama.

Ameyasema hayo wakati akiwaapisha wajumbe wa Kamati ya Maadili ya Maafisa wa Mahakama ngazi ya Mkoa katika ukumbi wa Manispaa mjini Songea.

Amewakumbusha wajumbe hao kuwa chimbuko la viapo vyao ni kanuni za uendeshaji wa kamati za maadili za maafisa wa Mahakama kwa ngazi ya Mkoa na Wilaya.

"Kiapo hiki kinawafanya wajumbe wawajibike kwa kuwakumbusha kila mmoja kuyazingatia aliyoapa, kwa kumtanguliza Mungu na kutenda haki bila chuki, huba wala upendeleo," alisema Jaji James.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amewashukuru na kuwapongeza wajumbe wote wa kamati hiyo walioaminiwa na kupewa jukumu hilo kwa ngazi zote.

Ametoa rai kwa wajumbe hao kuendelea kutoa Elimu juu ya uwepo wa kamati na majukumu yake ili kuwasaidia wananchi kuwasilisha malalamiko yao na kufanyiwa kazi.

"Mmeaminika, kazi zenu zinafahamika pia Serikali ya Mkoa na wananchi wana Imani na nyinyi hongereni sana," alisema Kanali Ahmed.

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Mary Makondo ameyataja matarajio ya wananchi ni kupata na kuifikia haki kupitia mifumo na Muundo wa Serikali hasa katika Muhimili wa Mahakama.



Kushoto ni Mkuu Wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed akiwa na Jaji Mfawidhi, Mahakama Kuu ya Tanzania kanda ya Songea Mheshimiwa James Karayemaha

# ELIMU YA WATU WAZIMA ITILIWE MKAZO-RAS RUVUMA



Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Bi. Mary Makondo, amesisitiza umuhimu wa maandalizi ya rasilimali watu ili kukuza uchumi wa nchi ambapo amesema ni muhimu kutoa maarifa na ujuzi kwa watu wote ili kuleta ustawi katika jamii.

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho ya Juma la Elimu ya watu wazima, ambayo kimkoa imeadhimishwa Wilayani Nyasa, Bi. Mary amesema Nchi yoyote duniani bila kuwa na rasilimali watu ambayo imeandaliwa vema, vigezo vingine haviwezi kuwa na manufaa na maendeleo yanaweza kuwa ni ndoto.

Amebainisha kuwa bado jitihada zinahitajika ili kuongeza idadi ya wanafunzi na kuimarisha Elimu ya watu wazima kama ilivyo dhamira ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kila msichana aliyekatisha masomo anarejeshwa shuleni.

“Niwaombe ndugu zangu wa Taasisi ya Elimu ya watu wazima Mkoa wa Ruvuma kusimamia uwepo wa madarasa ya kutosha kupitia mradi wa SEQUIP na kuona umuhimu wa mtoto wa kike anamaliza masomo yake licha ya changamoto anazopitia,” alisema Bi. Mary.

Bi. Mary ametoa rai kwa wakurugenzi wa Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma, maafisa Elimu msingi na sekondari kuhakikisha kuwa Elimu ya watu wazima inatiliwa mkazo kwa kuweka mikakati mizuri ili iweze kutekelezwa vizuri zaidi ya hivi sasa.

Nae Mkuu wa Wilaya ya Nyasa Mhe. Peres Magiri amewataka wanafunzi waliopo katika mradi wa Elimu ya watu wazima kuitumia fursa hiyo vizuri kwa kuwa

wanaweza kufanya vizuri na kuwa msaada mkubwa katika maisha yao na jamii kwa ujumla.

Amewashukuru wadau wa Elimu wanaoshirikianana nao na kuwasisitiza wote wanaoshiriki mradi huo ikiwa ni pamoja na walimu kuendelea kutimiza wajibu wao.

Juma la Elimu ya watu wazima ni maadhimisho ya kusherehekea maendeleo na mafanikio ya Elimu ya watu wazima nchini na kufanya tathmini ya shughuli za Elimu ya watu wazima zinazotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mzima.

## BILIONI 1.7 ZATEKELEZA MRADI WA MAJI MBINGA



WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini(RUWASA)wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma,umeanza kutekeleza mradi wa maji ya bomba wa Kitula kata ya Kitula Halmashauri ya wilaya Mbinga utakaowaondolea wananchi wa kata hiyo kero ya kuamka usiku wa manane na kutembea umbali mrefu kila siku kwenda kutafuta maji na kuacha shughuli za kujipatia kipato.

Meneja wa RUWASA wilaya ya Mbinga Mhandisi Mashaka Sinkala amesema,mradi wa maji Kitula unatekelezwa kwa gharama ya Sh.bilioni 1.7 na

utawanufaisha wananchi 9,100 wa vijiji vinne vya Mzuzu,Kitula,Mahilo na Lisau na utekelezaji wake umefikia zaidi ya asilimia 85.

Sinkala ametaja kazi zinazofanyika katika mradi huo ni ujenzi wa matenki matatu moja la lita 150,000 la pili la ujazo wa lita 100,000 la tatu lina uwezo wa kuhifadhi lita 75,000 na kulaza mabomba urefu kilometa 54.

Amesema, kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa matenki yote matatu na kujenga chanzo cha maji(Intake) na maji yameanza kufika kwenye matenki mawili kati ya matenki matatu kutoka kwenye chanzo.

Diwani wa Kata ya Kitula Mheshimiwa Alex Ngui amesema,mradi huo umewasaidia sana wananchi wa kata hiyo kupata huduma ya maji safi na salama kwenye maeneo yao na hivyo kupata muda mwingi wa kushiriki kazi mbalimbali za maendeleo.

Ngui amemshukuru Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo kwa kuwa utaleta tija kubwa kwa wananchi na kuharakisha maendeleo ya mtu mmoja mmoja,wilaya ya Mbinga na mkoa wa Ruvuma hasa ikizingatia kuwa wananchi wa kata hiyo ni wakulima wakubwa wa zao la kahawa linalohitaji maji mengi.

## LITUMBANDYOSI WAFURAHIA KITUO KIPYA CHA AFYA




WAKAZI wa kata ya Litumbandyosi Halmashauri ya wilaya Mbinga mkoani Ruvuma,wameondokana na adha ya kutembea umbali wa kilometa 85 kufuata

huduma za afya Mbinga mjini baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha afya Litumbandyosi kilichogharimu Sh.milioni 500.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya wilaya Mbinga Dkt Seleman Jumbe amesema,kituo hicho kimejengwa kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri ya wilaya ni kinahudumia zaidi ya wakazi 15,000 wa kata ya Litumbandyosi na maeneo ya jirani.

Dkt Jumbe ametaja majengo yaliyojengwa katika kituo hicho ni jengo la wagonjwa wa nje(OPD)maabara,wodi ya wazazi kwa ajili ya kulaza na kujifungua,jengo la kufulia nguo,kichomea taka na kufunga jenereta.

“Sisi kama Halmashauri ya wilaya Mbinga tunaishukuru Serikali,wananchi wa kata ya Litumbandyosi na vijiji vya jirani wamepata msaada mkubwa kwa kuwepo kwa kituo hiki kwani kimesaidia wananchi kutoangaika tena kwa kwenda maeneo ya mbali kufuata huduma za matibabu”alisema Dkt Jumbe.

Kwa mujibu wa Dkt Jumbe,tangu kituo kilipofunguliwa mwezi mei mwaka huu kimesaidia sana kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto kwani hapo awali baadhi ya mama hao walipoteza maisha njiani kabla ya kufika kwenye maeneo ya kutolea huduma za afya.




Jengo la wazazi katika kituo cha afya Litumbandyosi Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma

# MAELEKEZO MUHIMU YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024



Uchaguzi wa serikali za mitaa unatarajia kufanyika **tarehe 27 Novemba, 2024**. ambapo Mkoa wa Ruvuma una jumla ya Kata 173, Vijiji 551 Mitaa 123, Vitongoji 3,691 na mamlaka za miji midogo miwili ambayo ni .mamlaka ya Mji mdogo wa Namtumbo na Lusewa,ambavyo vitashiriki katika uchaguzi wa kuwapata viongozi katika ngazi ya mitaa,vijiji na vitongoji.

# BILIONI 18.5 KUJENGA CHUO KIKUU SONGEA




Meneja wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) Tawi la Songea Dkt. Bakari Mashaka amebainisha kuwa chuo hicho kinaleta mradi Mkubwa wa bilioni 18.5 za Kitanzania ambazo ni fedha za Serikali kujenga Chuo Kikuu Katika Mtaa wa Pambazuko kata ya Tanga Manispaa ya Songea.

Ameeleza hayo katika hafla ya ugawaji wa vifaa vya Michezo ambapo Chuo Kikuu hicho kimetoa mipira ya Miguu saba kwa timu za mpira wa Miguu zilizopo katika mtaa wa Pambazuko Kata ya Tanga, Manispaa ya Songea.

"Tunaleta mradi Mkubwa wa takribani shilingi bilioni 18.5 za Kitanzania, ni fedha za Serikali kupitia Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu ambaye ameweka lengo Kila Mkoa uwe na Chuo Kikuu", alisema.

Amebainisha kuwa Chuo hicho kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kuchukua Wanafunzi kwa kuanzia 5,000 mpaka 10,000.

Sanjari na hayo ameeleza kuwa mradi huo utaanza kutekelezwa mapema kuanzia sasa mara baada ya taratibu za zabuni kukamilika na unatarajiwa kumalizika baada ya miezi 18.

Naye Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Pambazuko, Nickson Mhagama ameeleza kuwa wananchi wa Kijiji hiko wameupokea Mradi huo kwa furaha kubwa na wataendelea kushirikiana na Chuo katika utekelezaji wa mradi huo.

Ameushukuru uongozi wa Chuo Kikuu hicho kwa kuwaelimisha Wananchi juu ya faida za mradi huo.

Chuo Cha Uhasibu Arusha kina eneo lenye ukubwa wa takribani hekta 26.5 katika Mtaa wa Pambazuko kata ya Tanga Manispaa ya Songea ambapo ndipo mradi wa Tawi la Songea Meneja wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) Tawi la Songea Dkt. Bakari Meneja wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) Tawi la Songea Dkt. Bakari Mashaka

## RUVUMA KUELEKEA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA



Miongoni mwa wadau wa uchaguzi Zaidi ya 150 kutoka katika Wilaya zote mkoani Ruvuma wakiwa katika mafunzo ya maelekezo muhimu kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024 kilichofanyika kwenye ya ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea.



# RUVUMA ILIVYOJIPANGA KWA UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesema kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Novemba 11 mwaka huu kila mmoja ana wajibu wa kufanya kuhakikisha maandalizi yanakamilika kabla ya siku ya uchaguzi.

Kanali Ahmed ameyasema hayo wakati akizungumza na wadau wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika kikao kilichofanyika ndani ya ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

"Tukio ama shughuli mojawapo ni utoaji wa elimu au kuwapasha habari wananchi kuhusiana na zoezi hili na wajibu wao, hata kikao hiki ni sehemu muhimu ya maandalizi ya uchaguzi huu," alisema Kanali Ahmed.

Ameongeza kuwa tukio lingine ambalo litafanyika kabla ya uchaguzi ni uandikishaji wa wapiga kura ambao utaanza tarehe 11-20 Oktoba, 2024 hivyo amezitaka Wilaya zote na Halmashauri kuwahamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha.

"Sisi kama wadau ni muhimu tushirikiane kuhakikisha eneo hili linafanikiwa, kama tukifanya vizuri katika maeneo haya matukio mengine ya kampeni na siku ya kupiga kura yatafanyika vizuri,"alisema.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Bi. Mary Makondo amesema wote kama wadau wanapaswa kushirikiana kuwahimiza wananchi wajitokeze kujiandikisha ili wapate sifa za kupiga kura.

Kwa upande wake Mratibu wa uchaguzi wa Mkoa wa Ruvuma Salum Kateula amesema lengo la kikao hicho ni kupitia maeneo muhimu yanayohusu kanuni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka 2024.

Ameongeza kuwa wananchi wanaendelea kuelimishwa kuhusu uchaguzi kwa kutumia mabango, matangazo, matamasha, na vikao mbalimbali katika ngazi za Wilaya, kata, na vijiji ambapo Elimu hiyo inalenga kuwawezesha kujiandikisha katika daftari la wapiga kura na kuelewa mchakato mzima hadi siku ya uchaguzi.

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mara ya mwisho ulifanyika tarehe 24 Novemba, 2019 ambapo mwaka huu uchaguzi huo unatarajiwa kufanyika tarehe 27 Novemba.

## IJUE HIFADHI YA MSITU WA WINO MADABA



Hifadhi ya msitu wa Wino iliyopo katika Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma ni miongoni mwa mashamba 24 ya miti ya kupandwa yanayosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

Hifadhi hii kwa sasa ina ukubwa wa hekta 39,718 zinazoundwa na safu tatu (Wino 2,259ha, Ifinga 29,000ha na Mkongotema 8,459ha).

Mhifadhi Mkuu wa Shamba miti Wino Glory Kasmiri anasema uhifadhi ya msitu wa Wino ulianza kuendelezwa na TFS mwaka 2010 ikihusisha eneo dogo la msitu wa asili wenye ukubwa wa hekta 2,259 (ambayo ndio safu ya Wino).

“baadae mwaka 2014 na 2016 tulipata maeneo kutoka vijiji vya Mkongotema na Ifinga , tangu tumeanza upandaji wa miti mpaka sasa jumla ya hekta 5,495 zimepandwa miti ya jamii mbalimbali lakini sehemu kubwa ikiwa ni misindano’’,anasema Kasimir

Anabainisha kuwa shamba la miti Wino limeendelea kuboresha mahusiano na wananchi,na kwamba katika kutekeleza hayo Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kupitia Shamba la miti Wino uliridhia na kufadhili mradi wa maji kijiji cha Ifinga uliogharimu Zaidi ya milioni 482.

Ametoa rai kwa wananchi na jamii kutunza mradi huu na maeneo yote ya vyanzo vya maji ili kuhakikisha upatikanaji wa maji unakuwa endelevu.

Anayataja malengo makuu ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya msitu wa Wino ni pamoja na:Kuhifadhi maliasili zinazotaka kutoweka na vyanzo vya maji, Vyanzo vya mto upahila – lutukila-luhuhu-Ziwa Nyasa,Mto Mnywa masi – Pitu-Ruhuji-ifakara-Rufiji,Mto Mwesa – Ruhuji na Mto Lutukila – Luhuhu.

Mito mingine ni Mgombezi – Lutukila,Mto Kineneka – Lutukila,Mto Kipilili – Pitu,Mto Balali – Pitu,Mto Mapancha – Chechengu-pitu,Mto Mbega – Chechengu na Mto Chechengu – Pitu

Malengo mengine ya kuanzishwa kwa shamba hilo ameyataja kuwa ni kutoa ajira kwa Watumishi wa kudumu 15, mkataba 10, vibarua wa msimu wanakadiriwa kufikia 4,000,Mazao ya biashara kama mbao na nguzo za umeme kwa siku za usoni ili kuongeza mapato ya serikali n Kuboresha mazingira na hali nzuri ya hewa . Akizungumzia shughuli za upandaji miti katika Shamba la miti Wino,Meneja huyo anasema upandaji miti unaeendelea kufanyika kwa lengo la kuhakikisha uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji vinatunzwa vizuri kwa upatikanaji maji na mazao ya Misitu kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Hata hivyo ameitaja changamoto ya matukio ya moto kwa kiasi kikubwa hupunguza jitihada za usimamizi endelevu wa shamba. Vyanzo vikuu vya moto ni uandaaji wa mashamba msimu wa kilimo kwa kutumia moto ambapo kwa mwaka 2016 ziliungua hekta 600 na 2021 hekta 1,623 ukisababishwa na uaandaaji wa mashamba maeneo ya mabonde yanayopakana na Shamba.

Katika kukabiliana na tatizo hili, Uongozi wa Shamba la miti wino umekuwa ukitoa elimu na vifaa vya kuzimia moto kwa jamii,kutoa msaada wa vitendea kazi vinavyotumika kuzimia moto kwa jamii,kujenga mahusiano mema na vijiji vinavyozunguka Shamba kwa kuwapatia vifaa vya ujenzi mbalimbali.

Hatua nyingine zinazochukuliwa amezitaja kuwa ni kufanya kazi za kinga dhidi ya moto (kusafisha Fire lines na kufungua barabara, Kufyekea miti, uwepo wa vituo 3 vya mawasiliano, doria ya msituni mwaka mzima, kuimarisha ulinzi wa kupambana na moto kipindi chote cha kiangazi, kuweka gari standby kwa kiangazi na mfumo wa satelaiti wa kuangalia matukio ya moto uliopo makao makuu ya Wakala.

“Shamba la miti Wino linaendelea kuwaomba wananchi kuepuka kuanzisha moto maeneo hatarishi wakati wa uandaaji wa mashamba na kuwataka kufanya maandalizi mazuri ya barabara za kinga moto’’,anasema.

Licha ya changamoto hizo Shamba la Miti Wino limeweza kufanikiwa kuhifadhi eneo,miti iliopandwa imestawi vizuri,TFS kupitia shamba hili imeimarisha ushirikiano wake na jamii na uongozi katika ngazi mbalimbali,shamba limetoa

ajira miaka yote kwa makundi mbalimbali. Kwa wastani wananchi 4,000 hujipatia ajira za mda mrefu na mfupi katika shamba hili kwa mwaka.

Anasema shamba hilo pia limevutia wawekezaji wengine kuja eneo hili,kikiwemo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ambapo pia wamepewa ardhi na kijiji cha Ifinga.

Anaitaja mipango ya baadaye ya shamba hilo ni kuhakikisha kwamba mazingira yanatunzwa ipasavyo na upatikanaji wa malighafi kwa viwanda vya misitu na watumiaji wengine unakua endelevu kwa kizazi kilichopo na kijacho.

## MAFUNZO YA MAAFISA UANDIKISHAJI MBINGA



Maafisa uandikishaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma wamepatiwa mafunzo juu ya zoezi la uandikishaji wa orodha ya wapiga kura katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika tarehe 27 Novemba 2024.

Pamoja na mafunzo hayo maafisa hao wamepata kiapo cha uaminifu, utii na uadilifu katika kutimiza majukumu yao.

# CRBD YAWAPIGA JEKI WANAFUNZI TUNDURU




BENKI ya CRDB Kanda ya Kusini,imetoa msaada wa meza 40 na viti 40 vyenye thamani ya Sh.milioni tatu katika shule ya Sekondari Kungu iliyopo kata ya Nakayaya Halmashauri ya wilaya Tunduru mkoani Ruvuma ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Serikali ya awamu ya sita ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Meneja wa CRDB Kanda ya Kusini Daniel Mwoleka amesema,wameamua kutoa msaada huo ili kurudisha faida kwa wadau wake kwani kuna kila sababu ya kusaidia shughuli mbalimbali za maendeleo zinazofanywa na Serikali.

“Benki ya CRDB kama mdau mkubwa wa elimu tunayo furaha kuwepo mahali hapa kwa ajili ya kutoa mchango wetu kwa ajili ya shule hii,kama nilivyosema sisi ni mdau wakubwa wa elimu”alisema Mwoleka.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shule hiyo Ismail Hamis Seleman, ameishukuru benki ya CRBD kwa msaada huo ambao utapunguza uhaba wa vifaa katika shule hiyo ambayo ina miaka miwili tu tangu kuanzishwa kwake.

# RAS RUVUMA ATAHADHARISHA UTOAJI TAKWIMU ZISIZO SAHIHI



Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Bi. Mary Makondo ametahadharisha kuwa takwimu zisizo sahihi zinaweza kusababisha upotevu wa rasilimali na kuchelewesha maendeleo yanayotakiwa kuonekana katika jamii

Ameyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya Mfumo wa fursa na vikwazo kwa maendeleo (O&OD) Ulioboreshwa kwa Waratibu wa Mfumo huo kwa Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma yaliyofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

"Takwimu zisizo sahihi zinaweza kusababisha upotevu wa rasilimali na kuchelewesha maendeleo tunayotamani kuyaona katika jamii", Alisema.

Amewataka Waratibu hao kutoa takwimu sahihi na kufanya kazi ili kuwa na taarifa zilizo sahihi kwani matarajio kuanzia ngazi ya Taifa hadi Msingi ni makubwa na wananchi wanahitaji maendeleo.

Amewaagiza wataratibu kuandaa taarifa mapema, kuzikamilisha na kuziwasilisha kwa wakati na kufanya kazi kwa weledi kwani bila ya kuwa na taarifa ni sawa na kutokufanya kazi na kushindwa kuwajibika jambo ambalo ni kosa.

Ametoa rai kwa Waratibu hao kuacha kufanya kazi kwa mazoea kwani hali hiyo inachelewesha kufikiwa kwa malengo ya Serikali na kuwakosesha Wananchi maendeleo na kuwataka kubadilika na kujipanga vyema kufanya kazi kwa ufanisi.

Sanjari na hayo ameeleza kuwa Mfumo wa fursa na vikwazo ulioboreshwa ni moja ya juhudi zinazofanywa na Serikali kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wananchi ili Kuwaongezea ari ya ushiriki kwa kupanga na kusimamia shughuli za maendeleo.

Amelitaja lengo la maboresho ya Mfumo huo kuwa ni kuhakikisha wanaweza kutatua changamoto zilizokuwa katika mfumo wa awali,

## RC RUVUMA AKABIDHIWA MAKOMBE MANNE YA KITAIFA



klabu ya RAS Ruvuma imekabidhi jumla ya makombe manne kwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed iliyoyapata katika Mashindano ya Shirikisho la Michezo(SHIMIWI) Taifa yaliyofanyika Mkoani Morogoro.

Akizungumza wakati wa tukio la kukabidhiwa makombe hayo Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed ameipongeza klabu hiyo kwa kuwa na mipango na mikakati iliyowezesha kupata ushindi wa makombe na medali hizo.



# RC RUVUMA AWAONGOZA WANANCHI SONGEA KUJIANDIKISHA




Pichani ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed akijiandikisha katika daftari la Wapiga kura katika kituo cha Mtaa wa Mahenge Kata ya Mjini Halmashauri ya Manispaa ya Songea.Zoezi la kujikiandikisha litawezesha wananchi kushiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika Novemba 27 mwaka huu.



## WANANCHI RUVUMA WAASWA KUJITOKEZA KUJIANDIKISHA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amewaasa wadau na wananchi kujitokeza kwenye zoezi la uandikishaji wapiga kura ambalo linafanyika kwa siku kumi kuanza Oktoba 11 hadi 20 mwaka huu.

Kanali Abbas Ametoa rai hiyo wakati anafungua kikao cha wadau wa uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2024 kilichofanyika kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea .

“Sina shaka kila mmoja wetu anajua kuwa mafanikio ya uchaguzi huu yanategemea sana ni kwa kiwango gani wananchi wetu watakuwa wamejiandikisha,matarajio yangu ni kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Songea mtahamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha ili wananchi wote wajiandikishe’’,alisisitiza.

Amewaasa wadau wa uchaguzi kuhakikisha eneo hilo linafanikiwa hali ambayo itawezesha maeneo mengine ya kampeni na siku ya kupiga kura kupata mafanikio mazuri.

Katika kikao hicho wadau muhimu wakiwemo maafisa watendaji wa mitaa na kata kutoka Manispaa ya Songea wameshiriki,ambapo Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma amewaasa watendaji hao kuhakikisha wanakuwa waadilifu katika kazi hiyo na kufanya kazi kwa kuzingatia kanuni na miongozo ya uchaguzi.

Kanali Abbas amewatahadharisha watendaji hao kujiepusha na tabia zinazoweza kusababisha kuwa wazembe ili kazi hiyo iweze kufanyika kikamilifu kama ilivyotarajiwa.

# MAHAKIMU RUVUMA WAPATA MAFUNZO YA UCHAGUZI




Mahakama Kuu Kanda ya Songea imetoa mafunzo ya uchaguzi wa serikali za mitaa kwa waheshimiwa mahakimu wakazi kutoka Wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma.

Mafunzo hayo ya siku moja yamefanyika kwenye ukumbi wa hoteli ya Huntlcub Ruhuwiko mjini Songea,yamefunguliwa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Songea Mheshimiwa James Karayemaha.

Akizungumza kwenye ufunguzi wa mafunzo hayo,Jaji Mheshimiwa Karayemaha amesema Mahakama hiyo iliandaa sera ya mafunzo ya mwaka 2019 kwa lengo la kushusha mafunzo kwenye Kanda hiyo.

Amesema mafunzo hayo yameandaliwa kama sehemu ya utekelezaji wa sera hiyo ambayo yatawajengea uwezo waheshimiwa mahakimu kufahamu sheria mbalimbali zinazohusiana na uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa kwa mwaka 2024.

“Mafunzo ya uchaguzi wa serikali za mitaa ,yatawasaidia kujua sheria,kanuni na taratibu zinazoongoza uchaguzi,yatasaidia kujua namna bora ya kupokea ,kusikiliza na kuamua migogoro ya aina yoyote itakayoletwa mbele ya mahakimu’’,alisisitiza.

Hata hivyo ameutaja uchaguzi wa serikali za mitaa ni suala muhimu katika ustawi wa demokrasia nchini ambapo waheshimiwa mahakimu wote wa Tanzania ni

sehemu ya mchakato wa kufanikisha uchaguzi wa serikali za mitaa ambao ni makamishina wa viapo.

Amewataja waheshimiwa mahakimu kuwa ndiyo watakaowaapisha wasimamizi wa uchaguzi na viongozi watakaochaguliwa kabla ya kuanza rasmi kufanya shughuli zao kwa mujibu wa sheria.

Katika hatua nyingine Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Songea amewahimiza watumishi wa Mahakamu kufanya kazi kwa kusikiliza na kutoa maamuzi kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEHAMA hivyo kuachana na matumizi ya karatasi.

Kwa upande wake Mwezeshaji wa mafunzo hayo Hakimu Mkazi Mfawidhi,Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Songea Mheshimiwa Japhet Manyama amesema mafunzo hayo yanatolewa kwa waheshimiwa mahakimu kwa lengo la kuwaandaa kwa ajili ya kusikiliza na kuamua mashauri yatakayotokea wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa.

Amelitaja lengo kuu la mafunzo hayo kuwa ni kuwaandaa na kuwapitisha mahakimu katika sheria zinazohusu uchaguzi zikiwemo kanuni zinazotumika kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na kuwaandaa namna ya kumudu msukumo wa kisiasa na jamii kwa kuangalia sheria ili waweze kutoa maamuzi ya haki kwa wote.



Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Songea Mheshimiwa James Karayemaha

# MBUNGE ASHAURI WANANCHI KUJITOKEZA KUJIANDIKISHA



Naibu Waziri Nishati na Mbunge wa Viti Maalum Vijana Taifa, Mhe. Judith Kapinga amewahamasisha wananchi katika Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma kujitokeza kwa wingi katika zoezi la kujiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili waweze kuchagua viongozi watakaowaletea maendeleo.

Mhe. Kapinga amesema hayo wakati akifungua Mafunzo ya Matumizi ya Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 kwa Viongozi, Watendaji na Wadau wa Wilaya ya Mbinga.

“Ni muhimu kila mmoja wetu akashiriki zoezi la kujiandikisha, sio kujiandikisha wewe tu bali kuhamasisha na wengine kwenye eneo lako waweze kujiandikisha.” Ameeleza Kapinga

Amesema ili wananchi waweze kuweka viongozi imara watakaofaa kwenye jamii, ni lazima kuwe na watu wengi wa kuwapigia kura, hivyo ni vyema wananchi wakahamasishana ili kwenda kwa wingi kujisajili kwenye daftari la kudumu la wapiga kura.

Aidha, ametoa rai kwa wananchi kuchagua viongozi watakaowatumikia kwa weledi na kutatua changamoto mbalimbali pale zinapojitokeza.

## ROBO TATU YA WILAYA YA NAMTUMBO NI HIFADHI



Utafiti umebaini kuwa robo tatu ya wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma ni hifadhi ikiwemo eneo la Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

Katika shoroba unayounganisha Selous na Niassa nchini Msumbiji kuna hifadhi tatu ndani ya Wilaya ya Namtumbo ambazo ni Mbarang'andu, Kisungule na Kimbanda.

Wilaya ya Namtumbo inahusika katika mradi mkubwa wa umeme wa Rufiji unaoendelea kutekelezwa na serikali ya Awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan.

Mto Luegu unaonzia Wilaya ya Namtumbo unachangia asilimia 19 ya maji katika Mto Rufiji.

Jumuiya ya Hifadhi ya wanyamapori ya Mbarang'andu imekuwa kivutio kikubwa cha watalii kutoka nchi za Ulaya na Marekani ambao wanatembelea jumuiya hiyo yenye vijiji saba na kufanya aina ya utalii ambayo inahusisha moja kwa moja matumizi ya wanyamapori.

Jumuiya hiyo inahusisha vijiji saba ambavyo ni Mchomolo, Kitanda, Likuyuseka Maganga, Kilmasela, Nambecha, Songambele na Mtelemwahi.

# MKUU WA KAMANDI YA VIKOSI AZUNGUMZA NA RC RUVUMA




Mkuu wa Kamandi ya Vikosi Chini ya Makao ya Jeshi Meja Jenerali Idd Said Nkambi akizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed alipomtembelea ofisini kwake mjini Songea



# RC RUVUMA AHIMIZA KUIMARISHWA USHOROBA SELOUS NIASSA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesisitiza kuendelea kufanyiwa kazi kwa ushoroba wa Selous -Niassa ili kudhibiti muingiliano wa Wanyamapori wasilete madhara makubwa kwa Wananchi.

Kanali Ahmed ameyasema hayo alipokuwa akizindua mradi wa Global Biodiversity Framework, hafla iliyofanyika katika ukumbi wa Hunt Club Mjini Songea, Mkoani Ruvuma.

"Niendelee kusisitiza ushoroba huu wa Selous pamoja na Niassa ambao ni muunganiko mzuri baina yetu na Msumbiji, tuendelee kuufanyia kazi ili kudhibiti muingiliano wa Wanyamapori na Wanadamu ili wasilete madhara makubwa",Alisema.

Sanjari na hayo ameeleza jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuhakikisha Wanyamapori hawaleti madhara makubwa kwa nchi ikiwemo utoaji wa elimu, kufanya doria kwenye maeneo hatarishi, kuendelea kuwaandaa Askari Wanyamapori wa vijijini pamoja na kutumia ndege nyuki.

Naye Mkurugenzi wa Shirika la Kimataifa la Uifadhi wa Mazingira na Wanyamapori Duniani (WWF) Tanzania Dkt. Amani Ngusaru amebainisha Kusifika Kwa Tanzania Kikanda na Kimataifa kama Nchi yenye utajiri mkubwa wa bio-anuai.

Amesema Tanzania imetenga takribani asilimia 40 ya ardhi yake kwa ajiri ya uifadhi wa maliasili, misitu na Wanyamapori na kutokana na hilo Tanzania ni mojawapo ya Nchi 5 ambazo zimependekezwa na kupewa fursa ya kutekeleza mradi wa Global Biodiversity Framework.

## RC RUVUMA ALIVYOAGANA NA MKUU WA KAMANDI YA VIKOSI



Kushoto ni Mkuu wa Kamandi ya Vikosi Chini ya Makao Makuu ya Jeshi Meja Jenerali Idd Said Nkambi akiagana na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed baada ya kumtembelea oifisini kwake mjini Songea



# MKOA WA RUVUMA KUZALISHA KOROSHO TANI 28,000



Mkoa wa Ruvuma unatarajia kuzalisha na kuuza zao la korosho tani 28,000 katika msimu wa mwaka 2024/2025.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed wakati anazungumza kwenye uzinduzi wa masoko ya zao la korosho katika msimu wa mwaka 2024/2025 kwenye mkutano wa wadau wa tasnia ya korosho Mkoa wa Ruvuma uliofanyika kwenye ukumbi wa Skyway mjini Tunduru.

‘’Leo Oktoba 17,2024 tunafungua msimu masoko wa zao la korosho katika Mkoa wa Ruvuma,ni matarajio yangu kila mdau atashiriki vema kufanikisha msimu wa masoko ya zao la korosho’’,alisema.

Amesema katika msimu uliopita wa mwaka 2023/2024 Mkoa wa Ruvuma katika kutekeleza malengo ya kilimo cha zao la korosho ulizalisha jumla ya kilo milioni 26 sawa na asilimia 60.

Ili kuhakikisha zao la korosho linatoa mafanikio kwa mkulima,Mkuu wa Mkoa amekiagiza Chama Kikuu cha Ushirika Tunduru TAMCU kuhakikisha kinasimamia vizuri mfumo wa malipo kwa mkulima na kuhakikisha Halmashauri zinawasimamia maafisa ugani katika zoezi la ukusanyaji mazao.

Maagizo mengine ambayo ameyatoa Kanali Abbas ni Halmashauri na vyama vya ushirika kuhakikisha vinasajili wakulima kwa kuzingatia majina yao halisi,benki zinatumia majina kamili ya wakulima ili kufanya malipo

## RC RUVUMA AZINDUA MINADA YA KOROSHO



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amezindua minada ya zao la korosho kwa Mkoa wa Ruvuma.

Uzinduzi huo umefanyika katika kata ya Nakapanya ,Wilayani Tunduru Mkoani Ruvuma na kuhudhuriwa na wataalam, wadau pamoja na wakulima wa za hilo.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo Mkuu wa Mkoa amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuboresha sekta ya Kilimo.

"Niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya haswa kwenye Sekta ya Kilimo, sisi Mkoa wa Ruvuma tukiwa ni wanufaika wakubwa wa sekta hiyo", Alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho Tanzania Francis Alfred amebainisha kuwa bei zinazoendelea wakati huu katika Minada ndiyo bei zilizopo katika mwenendo wa Soko la Dunia.

Sanjari na hayo ameeleza kuwa Bodi ya Korosho ilitarajia mwenendo wa bei ya Korosho kwenye Soko la Dunia kuwa kati ya 3,000 Hadi 3,600 na ikizidi sana ni hadi 3,800.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Tunduru Mhe. Simon Chacha ameishukuru Serikali kwa kuweka jitihada kubwa za kuwasaidia Wananchi kwa kutoa Pembejeo kwa kiwango kikubwa.

## TAMASHA KUBWA LA TOYOTA KUFANYIKA NOVEMBA 22 HADI 23



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed, ametangaza tamasha la Ruvuma Toyota 2024 litakalofanyika Novemba 22 na 23 mwaka huu ambalo linalenga kuwahamasisha wananchi kuelekea uchaguzi wa Serikali za mitaa, utalii, uwekezaji na burudani.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye ukumbi wa Huntclub mjini Songea Kanali Ahmed Ameyataja malengo ya tamasha hilo ni kuwahamasisha wananchi kujitokeza kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kuufungua Mkoa katika sekta za utalili na uwekezaji na kuleta burudani.

"Tamasha la Toyota Festival 2024 kama Mkoa tumeliandaa kuhamasisha kuelekea kwenye uchaguzi wa Serikali za mitaa ili wananchi wajitokeze kwa wingi, kuendeleza jitihada za kuufungua Mkoa katika sekta za utalii na uwekezaji na kuleta burudani kwa wanaruvuma na mikoa jirani ambayo watapata fursa ya kushiriki," alisema Kanali Ahmed.

Amesema kuwa tamasha hilo litazinduliwa Novemba 22 kwa kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo maeneo ya jirani ndani ya Mkoa wa Ruvuma na kuhitimishwa Mbambabay wilayani Nyasa Novemba 23, ambapo kutakuwa na michezo mbalimbali ikiwemo kuogelea, kuvuta kamba, muziki na ngoma za asili.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Bi. Mary Makondo, amesema kuwa tamasha hilo litakuwa na manufaa kiuchumi na kijamii kwa Mkoa wa Ruvuma, watanzania na mwananchi mmoja mmoja.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Wategi Traders Company, Elizabeth Japheth, amemshukuru Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas kwa jitihada zake katika kuandaa Ruvuma Toyota Festival 2024 na ameikaribisha mikoa jirani kushiriki kwa kuwa lengo ni kuvitangaza vivutio vya utalii vinavyopatikana Mkoani Ruvuma.

Tamasha la Toyota 2024 linameandaliwa na Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Wategi Traders Company, ambalo linalenga kuhamasisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kukuza utalii na uwekezaji, na kutoa burudani kwa wakazi wa Ruvuma na mikoa jirani.

## RC APONGEZA UJENZI HOSPITALI YA MANISPAA SONGEA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amewapongeza wasimamizi wa mradi wa ujenzi wa hospitali ya Manispaa ya Songea iliyopo eneo la Sanangula, Kata ya Shule ya Tanga.

Ametoa pongezi hizo alipotembelea na kukagua maendeleo ya Hospitali hiyo ambapo amesisitiza umuhimu wa kuongeza kasi ya ujenzi na kuhakikisha kazi zinamalizika kwa wakati ili wananchi waweze kupata huduma za afya katika eneo la karibu.

"Nimekuja kuona utekelezaji wa miradi ndani ya Mkoa wetu wa Ruvuma ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwamba ikifika Disemba miradi mingi iliyopatiwa fedha iwe imekamilika," alisema Kanali Abbas

Amewataka watumishi wa hospitali hiyo kutoa huduma zinazolingana na taaluma yao kama wahudumu wa afya ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Amesisitiza kuwa mtaalam wa afya anatakiwa kuwa na huruma, kutoa huduma bora kwa wagonjwa na mwenye kujali, hivyo amewataka kuyazingatia hayo ili wananchi wanapoenda kupata huduma waone wapo kwenye eneo salama na sio eneo la manyanyaso.

Naye Mganga Mkuu wa Manispaa ya Songea Dr. Amos Mwenda amesema mradi huo ulianza kutekelezwa tarehe 9 Disemba 2021 na hadi kufikia Septemba 2024 Halmashauri ya Manispaa ya Songea imepokea Shiningi Bilioni 1.1 kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo.

Ameongeza kuwa mradi huo uliibuliwa na wananchi wa kata ya Shule ya Tanga kupitia mpango wa fursa na vikwazo ili kupunguza kero na umbali wa upatikanaji wa huduma za afya.

Awali wananchi wa kata ya Shule ya Tanga walilazimika kutembea kwa umbali wa kilometa 20 kufuata huduma za afya katika kituo cha afya cha Mjimwema na hospitali ya Rufaa ya Mkoa ,Songea,

## MADAKTARI BINGWA WA SAMIA WALIVYOFANYA KAZI RUVUMA




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesema huduma za kibingwa na ubingwa bobezi zinazotolewa na madaktari wa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni muhimu katika jamii kwani zinatoa nafasi kwa wananchi kupata huduma stahiki.

Ameyasema hayo wakati wa uzinduzi wa kambi ya matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi ya Dkt. Samia Suluhu Hassan awamu ya pili uliofanyika katika viwanja vya ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma.

"Ni ukweli usiopingika huduma hii ni muhimu kwa jamii yetu hasa kwa vituo vinavyotoa huduma katika ngazi ya afya ya msingi, matarajio yangu ni kuwa uwepo wenu katika kambi hii utatoa nafasi kwa wananchi kupata huduma stahiki," alisema Kanali Ahmed.

Ameongeza kuwa wataalam hao wataifanya kazi yao kwa ufanisi mkubwa, kwa kuwa Serikali imeboresha upatikanaji wa vifaa tiba na vituo vya kutolea huduma za afya vinaendelea kuboreshwa ikiwemo ujenzi na ukamilishwaji wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Hospitali za Halmashauri na Zahanati.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Dr. Louis Chomboko amebainisha kuwa madaktari hao watatoa huduma za kibingwa za magonjwa ya wanawake na ukunga, magonjwa ya ndani, magonjwa ya watoto na watoto wachanga, upasuaji na mfumo wa mkojo, mifupa na ajali pamoja na magonjwa ya kinywa na meno.

Dr. Chomboko amelitaja lengo la madaktari hao kufika mikoani ni kusogeza huduma kwa wananchi na kuendeleza dhana ya kupata huduma bora.

Kwa upande wake Dr. Philip Steven Muhonji akizungumza kwa niaba ya madaktari bingwa amesema wao kama wahudumu wa afya wapo tayari kutoa huduma ili kutimiza adhma ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA**
**Kupitia Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma**

**S.L.P 74 SONGEA**

**57180 RUVUMA**

**SIMU Nambari. 025-2602256/2602238**

**FAX Na. 2602144**

**E -MAIL:ras.ruvuma@tamisemi.go.tz**

**TOVUTI: www.ruvuma.go.tz**

**INSTAGRAM: rs ruvuma**

**FACEBOOK: rs ruvuma**

**YOUTUBE: rs ruvuma**